# DARASA LA NANE – KODI 001 – 2020

## KISWAHILI

### SEHEMU YA KWANZA
### LUGHA
### Muda: Saa 1 Dakika 40

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha kuchagua jibu lako lionyeshe katika **karatasi ya majibu** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.
3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

   **Namba Yako Ya Mtihani**
   **Jina Lako**
   **Jina La Shule Yako**
5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
7. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **moja** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano**

   **Katika Kijitabu cha Maswali:**

   21. Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
      A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo
      B. njuga, tari, kinubi, fidia
      C. harimuni, marimba, msondo, maleba
      D. siwa, zeze, upatu, nembo
      Jibu sahihi ni B

   **Katika Karatasi ya Majibu:**

   1. [A] [B] [C] [D] 11. [A] [B] [C] [D] 21. [A] [B] [C] [D] 31. [A] [B] [C] [D] 41. [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Swali 1 mpaka 15.**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15**. *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.*

Kilimo au zaraa kama __1__ ni ule __2__ wa mimea au __3__ wa wanyama na pia ndege. Mkulima anaweza kuwa __4__ wa kukuza mboga kama vile michicha, kabeji na __5__ au awe __6__ wa ufugaji wa ng'ombe, kondoo, mbuzi au ngamia kama __7__ ili __8__ matakwa yake. Mkulima stadi __9__ bila shaka __10__ siri maalum __11__ kazi yake. Yeye huelewa sana jinsi ya __12__ hali za anga na kujua wakati __13__ wa kulima, kupanda, kupalilia na ule wa __14__ mimea yake dawa __15__.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. kijulikanavyo | B. vijulikanavyo | C. iujulikanavyo | D. ijulikanavyo |
| **2.** | A. unawirishaji | B. ustawishaji | C. uendelezaji | D. upaliliaji |
| **3.** | A. ufungaji | B. ufujaji | C. ufugaji | D. ufuaji |
| **4.** | A. mhatari | B. mgwiji | C. hodari | D. zuzu |
| **5.** | A. nyinginezo | B. nyingine | C. mingine | D. mingineyo |
| **6.** | A. mjusi | B. mchuzi | C. mchuuzi | D. mjuzi |
| **7.** | A. kitegauchumi | B. kutegauchumi | C. kitekachumi | D. kitegaujumi |
| **8.** | A. kukithi | B. kukidhi | C. kudhiki | D. kuakisi |
| **9.** | A. wowote | B. yeyote | C. yoyote | D. lolote |
| **10.** | A. ataelewa | B. ameelewa | C. akaelewa | D. huelewa |
| **11.** | A. za | B. wa | C. la | D. cha |
| **12.** | A. kutabiri | B. kutambua | C. kuelezea | D. kubashiri |
| **13.** | A. afiki | B. muawana | C. mwafaka | D. nafaka |
| **14.** | A. kunyunyisa | B. kunyunyizia | C. kunyunyisha | D. kunyunyishia |
| **15.** | A. yafaayo | B. kifaacho | C. zilizofaa | D. zifaazo |

***Kutoka swali la 16 – 30, chagua jibu sahihi.***

**16.** Neno Ng'ombe lina sauti ngapi?
A. 5
B. 8
C. 4
D. 6

**17.** Wanyama alicheza vizuri kisha akatuzwa viatu vizuri. Neno vizuri limetaumika vipi?
A. Kivumishi, kielezi
B. Kielezi, kiwakilishi
C. Kielezi, kivumishi
D. Kivumishi, kiwakilishi

**18.** Wakati wa jua la utosi ni?
A. Alasiri
B. Adhuhuri
C. Machweo
D. Mafungianyama


**19.** Lipi ambalo ni neno baki katika orodha?
A. Wengu
B. Kongosho
C. Figo
D. Nyongani

**20.** Asha na Zawadi wameolewa na bwana Kasavuli hivyo Aisha na Zawadi wataitana?
A. Mwanyumba
B. Kivyere
C. Wakewenza
D. Mwamu

**21.** Kitenzi lia katika kauli ya kutendesha ni?
A. Lilisha
B. Lisha
C. Liliwa
D. Liza

**22.** Bunge la kitalfa liko mkabala wa bunge la Seneti. Maneno yaliyopigwa mstari ni?
A. Kihusishi
B. Kielezi
C, Kihisishi
D. Kiarifa

**23.** Maumbo yafuatayo ni?



A. Piashinda, duara, mwezi mwandamo
B. Ngoe, hilali, tao
C. Mstari sambamba, duaradufu hilali
D. Ngoe, geli, tao

**24.** Vijana wa mtaani waliambulia kufanya kazi ya msragambo. Maana ya kazi ya msragambo ni?
A. Kazi ya kibarua
B. Kazi ya suluhu
C. Kazi ya watu wengi
D. Kazi ya mapato madogo

**25.** Ipi katika sentensi zifuatazo iko katika wakati tegemezi ya kukanusha?
A. Yeye hupenda wali kwa kuku
B. Angewasili sherehe ingeanza
C. Asingetajwa asingetiwa mbaroni
D. Bi Maliwaza hatawasili leo

**26.** *Kanusha sentensi ifuatayo*
Alikuja akala
A. Hakuja na hakula
B. Alikuja lakini hakula
C. Hakuja na akala
D. Hakuja wala hakula

**27.** Majina haya yanapatikana katika ngeli gani?
Ukuta, waraka, unyusi, ubavu
A. U-YA
B. U-U
C. U-Zi
D. U-I

**28.** Chai ya mkandaa ni rangi ipi?
A. Hudhurungi
B. Zambarau
C. Nili
D. Waridi

**29.** Andika sentensi ifuatayo katika usemi taarifa
'Njoo hapa nikutume dukani,' mjomba alimwambia Kulecho
A. Mjomba alimwambia Kulecho njoo hapa nikutume dukani
B. Mjomba alimtaka Kulecho atumwe dukani
C. Mjomba alimwambia Kulecho aende pale atumwe dukani.
D. Mjomba alimwambia Kulecho atamtuma dukani pale

**30.** Nywele ziotazo katika mdomo na pua hasa kwa wanaume huitwa?
A. Sharafa
B. Masharubu
C. Nyusi
D. Kope

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40.***

Matumizi mabaya ya mazingira yameleta uharibifu mkubwa kwa mchanga. Matumizi hayo huuharibu udongo wa juu juu wenye rutuba na kuacha ukiwa tasa. Katika nchi yetu, takriban nusu ya nchi ni mazingira ya jangwajangwa. Watu waishio kwenye sehemu hizo ni 700,000 tu kutoka kwa jumla ya idadi ya kama 30,000,000. Wananchi wanaoishi huko ni wafugaji wa mifugo ambao huhamahama. Wengine huishi kwa kukusanya vyakula wanavyokula kutoka porini.

Makabila ya watu hao wanaoishi kwa kuhamahama bado wanafuata maisha yao ya kitamaduni ya tangu zama. Mojawapo ya makabila haya ni Warendile. Watu hawa hutembea mwendo wa kilomita kama hamsini kwa siku, pamoja na ngamia wao, wakitafuta malisho mapya. Ngamia hutoa maziwa kiasi cha mara tatu yale ya ng'ombe. Haya makabila hujitengenezea makao yaliyo rahisi kubomoa na kubebwa wakati wanapohama.

Kabila la Wasamburu hufuga ng'ombe. Ng'ombe na ngamia wana malisho tofauti. Ng'ombe hula nyasi nao ngamia hula majani ya miti kwa hivyo wanyama hawa hawashindanii malisho.

Mifugo hao ni kiini cha uchumi wa wafugaji hao. Huwapa maziwa, damu, nyama kwa chakula chao. Ngozi zao hutumiwa kwa kutengenza vibuyu hivyo vya kubebea maziwa au maji, mapambo na viatu. Nacho kinyesi chao hutumika kama kuni za kukoea moto na pia kwa kuezekea paa na kutunza nyumba zao sakafuni.

Hiyo ndiyo mazingira ya jangwa au nusu jangwa ya nchi yetu. Mtu anapoingia ndani zaidi anapambana na jangwa lenyewe hasa, ambapo mazingira ni kame.

Mazingira yawe ya jangwa au yasiwe hivyo, yote yanahitaji kutunzwa na binadamu. Watu wote wanastahili kuungana katika jambo hili kwa njia mbalimbali popote walipo na kwa wakati wote.

**31.** Sentensi ipi inaelezea jinsi mazingira yetu ni maisha yetu?
A. Mazingira yanayotegemea maisha
B. Viumbe vyote vinavyotunza maisha
C. Bila viumbe mazingira ni bure
D. Maisha ya viumbe hutegemea mazingira

**32.** Taja aina ya jangwa.
A. Jangwa la Suhara la Afrika
B. Jangwa la Barafu na Theluji duniani
C. Jangwa la Ukame na baridi kali
D. Jangwa la Warendille na Wasamburu

33. Kwenye majangwa makavu mvua hunyesha
A. baada ya muda
B. kwa nadra sana
C. mara kwa mara
D. kwa muda mrefu

34. Theluji na barafu hutokana na nini?
A. Joto na upepo
B. Ukame na joto
C. Baridi na maji
D. Upepo na ukame

35. Kutamalaki kwa jangwa ni?
A. Kupanuka
B. Kudidimia
C. Kupungua
D. Yote hayo

36. Ni kiumbe gani ambacho hudhuru mazingira zaidi kuliko vyote?
A. Mwanadamu
B. Ngamia
C. Mfugo
D. Ng'ombe

37. Kwa nini sehemu Fulani za Kenya zina msongamano wa watu ingawa nchi yetu ni kubwa?
A. Kwa vile watu ni wengi sana
B. Kwa sababu ardhi ni ndogo
C. Kwa kuwa watu wanahamahama
D. Kwa ajili sehemu kubwa ni jangwa

38. Wanyama wafugwao jangwani huwafaaje wafugaji wao?
A. Kwa kuhamahama
B. Kwa kubeba mizigo
C. Kwa chakula na mavazi
D. Kwa mapambo na viatu

39. Kwa nini makabila ya jangwani hayajengi nyumba za kudumu?
A. Hawana pesa za kutosha
B. Hufuata mila zao za kale
C. Hawakai mahali pamoja
D. Huishi kwa kutegemea mifugo

40. Kuna tofauti gani ya sehemu ya jangwajangwa na ile ya jangwa?
A. Sehemu moja ni kama zaidi ya ile nyingine
B. Jangwajangwa si kame kama jangwa
C. Jangwa ni kavu zaidi ya jangwajangwa
D. Hatujaambiwa

***Soma taarifa kifuatacho kisha ujibu maswali* 41 – 50.**

Vita vya kupambana na janga la UKIMWI ni vya watu wote duniani. Watu wote wanapaswa kushiriki ili kumshinda nduli huyu. Mapambano hayo ni ya namna mbalimbali.

Tutapambana na adui UKIMWI kwa njia ya kujielimisha kuhusu ueneaji wake, dalili zake na matibabu yake. Watu wote wameshaelezwa mengine juu ya hayo yote. Mapambano mengine muhimu sana ni kuhusu utunzaji wa wagonjwa wa'iolemewa na ugonjwa wa UKIMWI. Maadamu kwa sasa bado ugonjwa huu hauna dawa, ni wazi kuwa wale wote walioambukizwa, baadaye watazorotoka sana na kuhitaji msaada wa watu wengine.

Je utamsaidia mama au baba yako, dada au kaka, ndugu au jamaa, rafiki, jirani au mtoto wako? Watu hao wanakuhitaji katika muda huo wa mateso makali. Hatua ya kwanza ya kuwatunza wagonjwa hao ni kukaa nao na kuwaonyesha upendo na huruma. Tusiwaache peke yao. Tusiwatenge, tusiwalaumu. Tukae nao kulingana na maagizo ya daktari.

41. Vita vya kupambana na ugonjwa wa UKIMWI ni vya kina nani?
A. Vijana
B. Wazee
C. Wataalam wa afya
D. Binadamu wote ulimwenguni

42. Ushindi dhidi ya adui huyu utapatikana kwa njia zipi?
A. Kujulishana na kuelimishana
B. Kupendana na kutembeleana
C. Ushirikiano
D. Uelewano

43. Kufikia sasa ni idadi gani ya watu ambao hawajapata kusikia hatari zozote kuhusu janga la UKIMWI?
A. Hapana yeyote
B. Asilimia kumi
C. Pengine ni wachache sana
D. Takribani wote

44. Je dawa ya UKIMWI ni nini?
A. Sindano
B. Haijagunduliwa
C. Haijatayarishwa
D. Vidonge

45. Kuzoroteka ni kufanya nini?
A. Kuwa dhaifu
B. Kuwa mwembamba
C. Kukosa maarifa
D. Kukosa marafiki

46. Ni nani anaweza kuambukizwa UKIMWI?
A. Mtu wa makamu
B. Mtu yeyote
C. Vijana marafiki
D. Watoto wachanga

47. Kumwonyesha mgonjwa wa UKIMWI huruma na upendo ni kinyume cha hali gani?
A. Kumjali na kumsaidia
B. Kumtembelea na kumwamkua
C. Kumlaumu na kumlunza
D. Kumtenga na kumbagua

48. Chakula cha lishe ya hali ya juu ni kipi?
A. Ni cha kumfaa mwilini
B. Ni cha kumchangamsha
C. Ni cha kumwongezea damu
D. Ni cha bei ghali

49. Pamoja na matibabu na chakula ni uzingatiaji wa hali ipi unaoweza kumfanya mgonjwa ajiskie nafuu zaidi?
A. Mazungumzo
B. Usafi
C. Mapambo
D. Kimya

50. Ni nini maana ya heshima ya binadamu?
A. Kuwa mtu
B. Kujiskia mzima
C. Kutojichukia
D. Kutojiamini